Jamhuri Jumanne Januari 20, 2026 Pg 5

# LATRA mmeheshimisha abiria mwaka 2025

**DAR ES SALAAM**

NA KULWA **KAREDIA**

Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) imeheshimisha abiria. Hilo ndilo neno sahihi ambalo unaweza kulitumia popote ulipo wakati huu unapojiandaa kuuaga mwaka 2025 na kuukaribisha mwaka 2026.

Mamlaka hii mwaka huu imeweza kutokana na ukweli kuwa imefanya kile ambacho kila mwisho wa mwaka kimekuwa kikiwatesa wasafiri wanaotoka maeneo mbalimbali kwenda kwao kwa ajili ya kujumuika na familia zao wakati wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Kila mwishoni mwa mwaka maelfu ya Watanzania wamekuwa wakilia na kulizwa na wapiga debe na mawakala kutokana na kupandisha nauli wakati hakuna mabasi ya kutosha vituoni.

Tumeshuhudia wengi wao wakitapeliwa na kubaki wakilia wasijue cha kufanya. Mwaka huu imekuwa tofauti. Ni mwaka ambao abiria hawataisahau mamlaka yao kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya dhidi ya wasafirishaji.

Nianze kwa kusema Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Dk. Habib Suluo na timu yake kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wameonyesha hakuna kinachoshindikana mbele ya mamlaka ya serikali. Amehakikisha yuko mstari wa mbele kutoa elimu na kuwachukulia hatua kali mawakala na madereva wakorofi.

Tumeshuhudia usiku na mchana Dk. Suluo akiendelea na operesheni nzito na kuwakamata mawakala waliopandisha nauli kiholela, kuwakamata madereva ambao wanavunja sheria na madereva wanaotumia kilevi licha ya sheria kuwakataza.

Mwaka huu kwa mara ya kwanza mamlaka hii imefanikiwa kumkamata dereva wa serikali akiendesha gari wakati ana kilevi kingi mwilini kinyume cha sheria. Haya ni mafanikio makubwa.

Mafanikio haya yameleta mageuzi makubwa ndani ya Desemba na kuonyesha hakuna 'mkate mgumu mbele ya chai'. Mamlaka hii imeonyesha kila jambo linawezekana na inaweza kuwasimamia usiku na mchana Watanzania wakaepuka matatizo ambayo ni sugu kwao.

Wote tumekuwa mashuhuda wa hili. Dk. Suluo amelazimika kuacha kulala na kuvamia vituo vikubwa vya mabasi kama kile cha Magufuli, jijini Dar es Salaam. Huyu ni kiongozi wa aina yake ambaye anaonyesha kuguswa katika kutimiza majukumu yake.

Usiku na mchana Dk. Suluo na timu yake wanazunguka nchi nzima kupambana na madereva na wakala wasiotii sheria, matokeo yake hakika yanaonekana.

Hatua pia inatokana na mifumo mizuri ya mamlaka iliyowekwa mikoa mbalimbali ambayo inatimiza wajibu wake kwa wakati.

Maofisa wote wa mamlaka hii wamekuwa watumishi wema kwa kuwa wepesi wa kuchukua hatua pindi malalamiko yanapowafikia mezani, jambo ambalo linawafanya wawe karibu zaidi na wateja wao.

Katika Stendi ya Magufuli na maeneo mengine tumemshuhudia Dk. Suluo na timu yake wakiwanasa watu wasiotii sheria, huku akiwa na kazi moja muhimu ya kuwapa elimu abiria. Nasema mamlaka hii imewatendea haki abiria na Watanzania kwa ujumla.

Hadi tunafunga mwaka sijasikia kilio cha wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu wakilalamika, ukiacha abiria mmoja aliyetapeliwa nauli ya kwenda mkoani Katavi kwa kutozwa Sh 250,000. Hata hivyo wahusika wote wamekutana na mkono wa sheria.

Hili ni jambo la kujivunia kuona mamlaka ya serikali ikifanya kazi nzuri ya namna hii. Mamlaka hii imekuwa mstari wa mbele kuwahamasisha Watanzania kukata tiketi za kielektroniki ili kuwaepuka vishoka ambao wamezoea kuwaibia, kukata tiketi kwa njia ya mtandao na kutoa taarifa pindi wanapokutana na changamoto ya aina yoyote.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Suluo hakuishia hapo, aliamua kutoa vibali vya magari ya saizi ya kati kusafirisha Watanzania kwenda mikoani. Kitendo cha kutoa vibali vya muda kwa mabasi ya kati kumesaidia wananchi wengi kusafiri kwenda kwao.

Kutokana na mafanikio haya, ninatoa pongezi kwa Dk. Suluo na Kitengo cha Habari. Mmekuwa mfano wa kuigwa na taasisi zingine za umma, kwa kuwatendea haki Watanzania.

Mnatoa ushirikiano, iwe wakati wa mvua au jua. Mmekuwa wepesi kuwasilikiza wadau wenu wa sekta ya habari ambao wanapeleka taarifa zenu kwa jamii.

Nawasisitiza mipango hii mizuri mliyoweka mwaka 2025 iendelee hivyo hivyo mwaka 2026. Endeleeni kusimamia eneo hili kwa kuwasaidia wananchi wanyonge wanaoonewa na kundi la watu wachache.

Endeleeni kutoa elimu ya ukataji tiketi na mambo mengine muhimu. Kamateni mawakala wanaokiuka sheria. Kamateni madereva walevi na makondakta wa daladala katika miji mikubwa wanaopandisha nauli. Ndiyo maana mwaka huu mamlaka hii imekuwa mshindi wa kwanza katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi jijini Arusha. Kumbe inafanya mambo makubwa na mazuri.

Dk. Suluo na timu yako ninawatakia heri ya mwaka mpya. Mwendelee hivi hivi bila kulegeza kamba. Mmethubutu - mmeweza, hakuna kurudi nyuma. Tanzania itajengwa na Watanzania wenye moyo kama wewe na timu yako.

**0714207553, karediajibai@gmail.com**

CamScanner

Nipashe Jumanne Januari, 20, 2026 Pg 4

# Mabasi 49 yatua Dar kunusuru kilio cha mwendokasi

**Na Elizabeth Zaya**

JUMLA ya magari ya mwendokasi 49 yamewasili nchini na hivi karibuni yanatarajiwa kuanza kutumika kuongeza nguvu ya usafiri huo katika jiji la Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa uongozi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka(DART), magari hayo yatafanyakazi katika njia za Kimara-Gerezani, Kimara-Kivukoni na Kimara Morocco.

Aidha, magari 50 yapo kwenye meli na yatawasili wakati wowote wiki hii kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri.

Ikumbukwe kuwa, gari moja la mfano linalotumia mfumo wa gesi liliwasili Juni mwaka jana na kutumika katika njia ya Morocco-Kivukoni kwa majaribio kabla ya mengine kuwasili.

Kuwasili kwa mabasi hayo, kunakamilisha idadi ya mabasi 100 yaliyoahidiwa na serikali mwaka jana.

Mwaka jana, serikali iliahidi kuongeza mabasi mapya ikiwa ni miongoni mwa hatua inazochukua katika kuboresha usafiri wa umma katika jiji hilo la Dar es Salaam na kuleta unafuu kwa wananchi kwa kupunguza msongamano wa magari, kuokoa muda wa safari na kuongeza usalama wa uhakika wa usafiri.

Serikali ya Tanzania imeendelea na utekelezaji wa mradi wa mabasi ya mwendokasi katika jiji hilo la Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kupunguza msongamano wa magari na kuboresha huduma za usafiri wa umma.

Mradi huo ulianza kutekelezwa rasmi mwaka 2016, ambapo barabara ya Kimara hadi Kivukoni ilikamilika na kuwa sehemu ya huduma ya kwanza ya mabasi hayo na baadae kwenye barabara nyingine kuu nne.

Kwa sasa, mabasi ya mwendokasi yanatoa huduma katika barabara ya Kimara hadi Kivukoni, Ubungo hadi Gerezani, na Mbezi hadi Kivukoni na barabara ya Kilwa, huku ile ya Morocco ikiwa imesimama kwa muda baada ya kuharibiwa miundombinu yake katika purukushani za Oktoba 29 mwaka jana

Mabasi ya mwendokasi kwa kiasi kikubwa yamepunguza athari za usafiri kwa wananchi wa jiji hilo hususani katika njia ya Morogoro, ingawa bado kuna changamoto zinazohitaji kushughulikiwa ambazo zimekuwa zikitajwa mara kwa mara na watumiaji wa usafiri huo hasa wakililalamikia kukaa muda mrefu vituoni kusubiri mabasi.

Licha ya kupunguza ahueni ya usafiri ambayo imeletwa na huduma ya mabasi hayo, lakini usafiri huo umekuwa na nyakati za milima na mabonde katika utoaji wake wa huduma hiyo.

Mara kadhaa kutokana na malalamiko ya wananchi kuchelewa kufika vituoni, wamekuwa wakifikia hatua ya kujichukulia sheria mkononi baadhi yake yakipigwa mawe.

Mwaka jana tukio kama hilo la basi kupigwa mawe na wananchi, lilitokea katika kituo cha mabasi hayo cha Kimara ambacho ni miongoni mwa vinavyochukua abiria wengi kuliko ilivyo katika vituo vingine.

Baadhi ya sababu zilizochangia wananchi wa eneo hilo kuchukua hatua hiyo ya kupiga mawe, ni kuchelewa kufika vituoni na hivyo kusababisha msongamano mkubwa wa wananchi kusubiri kwa muda mrefu, nyingine ilikuwa kwa mabasi mengi yaliyoharibika yakiwa yameegeshwa kituoni huku wananchi 'wakisota' kwa zaidi ya saa moja wakisubiri usafiri.

> **"Mradi huo ulianza kutekelezwa rasmi mwaka 2016, ambapo barabara ya Kimara hadi Kivukoni ilikamilika na kuwa sehemu ya huduma ya kwanza ya mabasi hayo na baadae kwenye barabara nyingine kuu nne.**

Walidai kwamba hata yanapofika katika eneo hilo, usafiri huo uligeuka kama vita, kwa sababu kutokana na idadi kubwa ya watu, walikuwa wakigombania kuingia, wengine walilazimika kupitia dirishani na hivyo wezi nao wakitumia mwanya huo kuwaibia simu, fedha na mali nyingine huku wengine wakiumizwa, nguo zao zikiharibiwa au kuchafuliwa licha ya kwamba walikuwa wanawahi kwenye majukumu yao.

Tukio hilo lilimwibua mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam Albart Chalamila pamoja na aliyekuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwenda kuwasikiliza wananchi na kufikia hatua ya kutoa agizo la kuongezwa mabasi katika barabara hiyo kupunguza tatizo hilo.

Mikasa mingine ambayo imeyakumba mabas hayo ya mwendokasi tangu kuanza kutoa hudum ni kuingiliwa kwenye nji yake halisi na vyombo vingine vya usafiri n hivyo kusababisha ajali n uharibifu wa mabasi hayo na hivyo mengine kulazimika kusimama kw muda mrefu kutoa huduma kwa ajili ya matengenezo.

Kadhalika, mvua nayo ni miongoni mwa mikasa ya mara kwa mara ambayo imekuwa ikiikumba huduma hiyo ya usafir wa mwendokasi ambapo imekuwa ikijaa maji n hivyo kushindwa kuto huduma yake kwa ufanisi

Mkasa mwingine katik huduma hiyo ambao mpaka sasa bado athari zake hazijaisha ni lile tukio l mabasi kuchomwa moto lililotokea Oktoba mwak jana na waandamanaji.

Wandamanaji wali choma mabasi mawili n vituo 28 vya mwendokasi

CamScanner

Mwananchi Januari 20, 2026

# Sauti ya wananchi



## BARUA YA MSOMAJI

### Ujio wa mwendokasi Kimara tumaini jipya kwa wananchi

**Mhariri,**

Wakazi wa Kimara tumeteseka kwa muda mrefu na changamoto za usafiri wa mwendokasi, hivyo ujio wa mabasi mapya unatarajiwa kuleta ahueni kwa wananchi wanaosafiri kwenda katikati ya jiji kila siku kwa ajili ya kazi, biashara na shughuli nyingine za kiuchumi.

Imefikia hatua kwamba unapoamka asubuhi unaanza kuwaza kwanza utafikaje kazini, kutokana na vurugu na msongamano wa kugombania mabasi, hali inayosababisha ucheleweshaji na usumbufu mkubwa kwa wasafiri.

Hivi karibuni tumeona taarifa kuwa Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (Udart) imeleta mabasi mapya 49 yatakayoongeza uwezo wa usafiri katika barabara ya Kimara, jambo ambalo ni habari njema kwa wananchi.

Tumeambiwa mabasi hayo kwa sasa yapo katika karakana ya Dart Mbagala, jijini Dar es Salaam, yakifanyiwa maandalizi ya mwisho kabla ya kuanza kutoa huduma rasmi kwa wananchi.

Hata hivyo, kwa hali ilivyo sasa, tunatamani yaanze kufanya kazi haraka iwezekanavyo. Ombi langu kwa Serikali ni kuangalia uwezekano wa kuongeza mabasi mengine zaidi, kwa kuwa wakazi wa eneo hili ni wengi na wanategemea sana usafiri wa mwendokasi kwa shughuli zao za kila siku.

Pia, ni muhimu sisi wananchi kuyatunza mabasi haya ili yaendelee kutuhudumia kwa muda mrefu, kwani usafiri wa uhakika ni sehemu ya msingi ya maisha na ukuaji wa uchumi wetu.

Kwa upande wa viongozi na wasimamizi wa mabasi, tunasisitiza yafanyiwe matengenezo mara tu yanapoharibika, ili yasikae muda mrefu karakana, kwani hali hiyo hutukosesha usafiri na kuongeza mateso kwa wananchi.

**Msomaji**

Tuandikie barua yako kisha tutumie nasi tutachapisha kila siku kwenye kona hii.

**0765 864 917**